Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

# TANZANIA HEADS OF ISLAMIC SCHOOLS COUNCIL

## FORM TWO INTER ISLAMIC MOCK EXAMINATION

## KISWAHILI

**021**

**MUDA: SAA 2:30** **Jumatatu Septemba 10, 2018 mchana**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una jumla ya sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali 10.
2. Jibu maswali yote.
3. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Vifaa vyote vya mawasiliano haviruhusiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu ya upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |



www.africona.net

Pg (01) Africona

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

**SEHEMU A (Alama 15)**

**UFAHAMU NA UFUPISHO**

**1.** Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa makini, kisha jibu maswali yafuatayo:

Wazo la watu wengi juu ya muungwana ni kuwa **mtanashati** au kuwa ni asifu mwenye cheo kwa watu. Lakini nguo nzuri hazimtukuzi mtu wala hazimfanyi kuwa muungwana. **Tamathali** ya hili ni kwamba nguo ni kama ngozi ya mtu au manyoya. Ngozi ya simba haiwezi kumfanya punda kuwa simba. Uungwana wa kufanywa na mshoni ni mzaha, si uungwana wa kweli; neno muungwana lina maana kubwa zaidi kuliko nguo nzuri au adabu au elimu nzuri, kwa hakika kuhusiana hasa na **taamuli** au maadili kadhaa wa kadha ya akili na wema.

Kwanza muungwana hawezi kumuudhi mtu kwa neno au tendo lake, au hata kwa tazamo lake. Ana moyo wa utulivu, na anaweza kusisitiza kwa makini maoni ya watu wengine bila ya kujisibu kuwalazimisha wakubali maoni yake. Ni katimu, mnyofu na ni amini katika tabia yake kwa wengine. Kwa hivyo ni msikilizaji mwenye subira kuliko msomaji ajisifuye mwenyewe. Tabia yake ni jina na yu tayari kusaidia. Hana makuu wala **unafiki** yu mnyofu kwa kila asemalo au atendalo, **hajitwezi** kwa matendo yake wala hadumishi matendo ya watu wengine kwa sababu hana wivu. Humtakia heri kila mtu; hana undani na yeyote yule.

Muungwana asipodhuru mtu yeyote yule haoneshi kama hana nguvu ya kufanya dhara. Haudhi wala hadharau mtu yeyote kwa sababu ajua kwamba ushenzi kama huo ni kinyume cha uungwana. Ajua heshima ya mtu, naye humheshimu kila mtu.

Ana tabia njema kwa wengine na jamaa zake vile vile. Siku zote ni mwema kama baba. Mwaminifu kama rafiki na msaidizi kama ndugu. Hutenda na tena hujiendesha kama raia **mwadilifu** ajuaye kazi na madaraka yake kwa watu. Huchukuana na watumishi wake kwa mapenzi, huruma na upole. Hujiheshimu na kwa sababu hiyo, huwaheshimu wengine. Ni mwaminifu katika ahadi zake. Ahadi ya muungwana ndio mkataba wake na uungwana wa kweli.

**MASWALI:**

(i) Pendekeza kichwa cha habari kifaacho kwa habari hiyo (maneno matano).



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

(ii) Mwandishi asema “uungwana huhusiana hasa na taamuli au maadili kadha wa kadha ya akili na wema”. Hii ina maana kuwa;

(iii) Mwandishi anasema “Ahadi ya muungwana ndio mkataba wake”. Je maana ya maneno haya ni nini?

(iv) Eleza maana ya maneno yafuatayo yaliyokolezwa wino kwenye habari uliyoisoma.

(a) Hajitwezi

(b) Mwadilifu

(c) Mtanashati

(d) Tamathali:



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

________________________________________

(e) Unafiki

________________________________________
________________________________________
________________________________________

2. Andika ufupisho wa habari uliyosoma kwa maneno 50.

________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________
________________________________________

**SEHEMU B (Alama 20)**
**SARUFI**

3. (a) Kwa kutumia mifano dhihirisha dhima tano za viambishi awali.

(i) ________________________________________
________________________________________
Mfano ________________________________________

(ii) ________________________________________
________________________________________
Mfano ________________________________________

(iii) ________________________________________
________________________________________
Mfano ________________________________________

(iv) ________________________________________
________________________________________
Mfano ________________________________________

(v) ________________________________________
________________________________________



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers



Mfano ______________________________________________

(b) Tunga sentensi kwa kutumia aina za maneno zifuatazo:
Mfano: Jana usiku litumike kama kielezi.
- Wote wawili waliondoka jana usiku.
Mimi litumke kama kiwakilishi.

(i) Mimi litumke kama kiwakilishi.

______________________________________________

(ii) Letu litumike kama kivumishi.

______________________________________________

(iii) Tutaendelea litumike kama kitenzi kisaidizi.

______________________________________________

(iv) Na litumike kama kiunganishi

______________________________________________

(v) Ndiye litumike kama kitenzi kishirikishi

______________________________________________

4. Panga maneno yafuatayo kama yanavyotakiwa kuwa katika Kamusi:

(a) Duwaa (a) ______________________
(b) Chichiri (b) ______________________
(c) Adhabu (c) ______________________
(d) Kidahizo (d) ______________________
(e) Faladi (e) ______________________
(f) Chege (f) ______________________
(g) Kitomeo (g) ______________________
(h) Dabiri (h) ______________________
(i) Anzali (i) ______________________
(j) Fanusi (j) ______________________

**SEHEMU C (Alama 20)**

**MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA**



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers



5. Andika maana mbili kwa kila moja ya sentensi zifuatazo:
   (a) Dada amechukua picha yangu.
   Maana ya kwanza ______________________________
   Maana ya pili ______________________________

   (b) Kaka alinipigia kura:
   Maana ya kwanza ______________________________
   Maana ya pili ______________________________

   (c) Tulishauriwa kupanda kilimani:
   Maana ya kwanza ______________________________
   Maana ya pili ______________________________

   (d) Mkaangie mwanangu
   Maana ya kwanza ______________________________
   Maana ya pili ______________________________

   (e) Tafadhali nipe sahani ya kulia
   Maana ya kwanza ______________________________
   Maana ya pili ______________________________

6. (a) Taja sehemu inakotumika kila moja ya rejesta zifuatazo:
   (i) Ndiyo afande! Nitawapeleka sasa hivi

   ______________________________

   (ii) Tumia moja kutwa mara tatu.

   ______________________________

   (iii) Kituo kinachofuata ni Mabibo Mwisho. Nani anashuka?

   ______________________________

   (iv) Okwi alimpiga chenga Jaja, hatimaye akaipatia Simba goli.

   ______________________________

   (v) Wapi supu! Nani chapati!



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers



______________________________________________________________

(b) Kwa kila kauli hapo chini andika KWELI kwa kauli ambayo ni sahihi na SI KWELI kwa kauli ambayo si sahihi mbele yake.

(i) Utumizi wa lugha hubadilika kutokana na muktadha, mada, wahusika na kusudio la mazungumzo. ________________________________________

(ii) Lugha ni sauti za nasibu zenye kubeba maana ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira husika. ____________________________________________

(iii) Lugha si lazima imhusu binadamu. ____________________________

(iv) Kutumia lugha fasaha katika mawasiliano si jambo muhimu. ____________

(v) Lafudhi ni utamkaji unaomtambulisha na kumtofautisha mtu na watu wengine. ___

**SEHEMU D (Alama 30)**

**FASIHI KWA UJUMLA**

7. (a) Malizia methali zifuatazo:

(i) Utajiri ni umande ______________________________________

(ii) Samaki mkunje ______________________________________

(iii) Msafiri ____________________________________________

(iv) Ajidhaniaye amesimama ________________________________

(v) Uzuri wa mkakasi _____________________________________

(b) Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo:

(i) Uhakiki ____________________________________________

(ii) Taswira ____________________________________________

(iii) Mtindo ____________________________________________

(iv) Dhamira ___________________________________________

(v) Migogoro ___________________________________________

8. Toa maana na mafunzo ya kila moja ya methali zifuatazo:



www.africona.net

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

(a) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
Maana ______________________________________________________________
Funzo ______________________________________________________________

(b) Haraka haraka haina baraka
Maana ______________________________________________________________
Funzo ______________________________________________________________

(c) Kikulacho ki nguoni mwako.
Maana ______________________________________________________________
Funzo ______________________________________________________________

(d) Mshika mbili moja humponyoka
Maana ______________________________________________________________
Funzo ______________________________________________________________

(e) Samaki mkunje angali mbichi.
Maana ______________________________________________________________
Funzo ______________________________________________________________

9. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuatia:

Nakuona waduwaa
Maisha kuyashangaa
Husda zimekujaa
Kuhusudu walojaa
Siharakishe maisha, nawe una fungu lako.

Ubado ni mwanafunzi
Usiingie simanzi
Ruka vikwazo vya panzi
Uipambe yako enzi
Maisha safari ndefu, kutembea usichoke.

Soma bado endelea
Sicheze pata potea
Muda ukishatimia
Maisha kufurahia
Usiache kutegua kwa kutegemea tega.

Punguza haraka zako

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers

Namba ya Mtahiniwa: ____________________

Badilisha mwendo wako
Subira ni chombo chako
Takutwisha kwenye fuko
Usisahau usemi subira yavuta kheri.

**MASWALI:**

(i) Nini dhamira kuu ya utungo huu?

______________________________________________

______________________________________

(ii) Kipi kinamkera mtunzi wa utungo huu?

______________________________________________

______________________________________

(iii) Taja ujumbe mmoja anaoutoa mtunzi:

______________________________________________

______________________________________

(iv) Ipi imani ya mtunzi juu ya maisha ya mtu?

______________________________________________

______________________________________

(v) Eleza fundisho moja unalolipata kutokana na utungo huu

______________________________________________

______________________________________

**SEHEMU E (Alama 15)**
**UANDISHI/UTUNGAJI**

10. Soma barua ifuatayo kwa makini kisha andika kadi ya mwaliko kwa Bwana Abu Ubaidah. Anwani yake ni S.L.P. 433 – IRINGA.

Shule ya Sekondari Maweni,
S.L.P. 126,
IRINGA.
16/5/2018.



www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers



Mpendwa Abu Ubaidah

Bila shaka hali yako ni njema pamoja na familia yako. Mimi pia sijambo, na tunawaandaa wanafunzi kufanya mtihani wa Taifa, mwezi wa Oktoba. Je wewe kazi zako zinaendeleaje?

Madhumuni ya barua hii ni kukutaarifu juu ya sherehe iliyoandaliwa na Shule kwa ajili ya kuwaaga wanaotarajia kuhitimu kidato cha nne. Sikukuu hiyo itafanyika tarehe 15/5/2018 kuanzia saa 4 asubuhi katika ukumbi wa Chuo cha Ualimu Makanya.

Wewe ni miongoni mwa wajumbe wa bodi ya shule hii, hivyo unaalikwa kushiriki siku hiyo muhimu. Kama hutahudhuria hafla hiyo, tafadhali ujulishe uongozi.

Nakutakia kazi njema

Ni mimi
Abulrahman Ibn Awf
MKUU WA SHULE



www.africona.net

## Wabillah Tawfiiq